

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**



TAARIFA KWA UMMA

**WAZIRI MKUU AIAGIZA NHC KUONGEZA NGUVUKAZI KATIKA UJENZI WA
MJI WA SERIKALI**

Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa, amemuagiza Mkandarasi anayesimamia ujenzi wa Ofisi mpya ya Wizara ya Fedha na Mipango kutoka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), kuhakikisha anaongeza rasilimali watu ili ujenzi huo ukamilike kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa .

Mhe. Majaliwa, ametoa agizo hilo wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Ofisi mbalimbali za Wizara katika mji wa Serikali eneo la Ihumwa Jijini Dodoma.

Alisema kuwa zimebaki siku 21 pekee kukamilisha ujenzi huo na lengo la Serikali ni kuona kazi hiyo imekamilika ifikapo Januari 31 mwaka huu, na akaonesha hofu yake iwapo ujenzi utakamilika kwa wakati kwa kuwa hakuridhishwa na nguvu kazi iliyopo.

“Mimi ninapokuta watu wachache huku kukiwa na kazi zisizohitaji kusubiri siku mbili kama kazi ya kuweka bimu, natarajia kuona watu wangukuwa wanaendelea kufanya kazi hizo”, alisema .

Aidha alisema kuwa Mawaziri kutembelea ujenzi unaoendelea na kuona ubora wa jengo ni jukumu lao na wanauwezo wa kuonesha kuridhika au kutoridhika na ujenzi huo.

Ameiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Wakala wa Misitu kuhakikisha mazingira ya eneo la Wizara linapandwa miti kulingana na ramani ya majengo ya muda na yakudumu.

Alisema kama watumishi waliopo ni wachache mkandarasi aongeze vijana ili ujenzi ukamilike mapema kwa kuwa kuna mafundi wengi Mkoani Dodoma na nje ya mkoa huo wanaotafuta kazi.

Kwa Upande wake Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji, ameahidi kusimamia maagizo ya Waziri Mkuu na kuhakikisha jengo linakamilika kwa wakati kwa kuwa hadi sasa asilimia 95 ya vifaa vyote muhimu vya ujenzi vimenunuliwa.

Akizungumzia suala la kuongeza nguvu kazi, Dkt. Kijaji, amesema Wizara itahakikisha Mkandarasi anaongeza nguvu kazi kwa haraka kutoka mtaani au Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ili ifikapo Januari 31 Wizara ikabidhiwe jengo rasmi.

Dkt. Kijaji alieleza kuwa Wizara ipo tayari kuhamia katika jengo hilo Februari mosi mwaka huu.

Naye Mhandisi kutoka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Elisante Olomi, anayesimamia ujenzi wa ofisi za Wizara hiyo, amesema ujenzi unaendelea vizuri na mpaka sasa umekamlika kwa asilimia 75, huku akiahidi kuongeza mafundi wakutosha.

Imetolewa na;

Benny Mwaipaja
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Fedha na Mipango